**HOTUBA YA UFUNGUZI YA MHE. JAJI FRANCIS S.K. MUTUNGI**

**MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

**KATIKA MAFUNZO YA VYAMA VYA SIASA KUHUSU UTEKELEZAJI WA SHERIA ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA MSAJILI**

**TAREHE 05 APRILI 2025 – UKUMBI WA HAZINA - WIZARA YA FEDHA, DAR ES SALAAM**

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Viongozi kutoka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa,

Ndugu Washiriki,

Mabibi na Mabwana,

Habari za asubuhi.... Jamhuri ya Muungano wa Tanzaniaa

Napenda kuwakaribisha kwa moyo wa dhati kwenye mafunzo haya muhimu yanayolenga kuimarisha uwezo wa vyama vyetu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kisheria, kiutawala, na kijamii.

Tunakutana leo kwa wakati muafaka, tukielekea katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, ambapo matarajio ya wananchi ni kuona ushindani wa haki, uwajibikaji wa kweli, na ushiriki wa kisiasa uliojengwa juu ya misingi ya sheria, maadili, na uzalendo.

Mafunzo haya yameandaliwa kwa makusudi mahsusi ya:

Kufafanua mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa (Sura 258) na Sheria ya Gharama za Uchaguzi (Sura 278);

Kuwezesha vyama kuwa na uelewa sahihi kuhusu uhakiki, usimamizi wa rasilimali, TEHAMA, na masuala ya fedha;

Kuhimiza uendeshaji wa ofisi za vyama kwa uwazi, na umuhimu wa kuzingatia kanuni za mawasiliano ya umma katika shughuli za vyama.

Mabibi na Mabwana,

Katika kipindi hiki tunachojifunza pamoja, nawasihi tutumie nafasi hii kuuliza, kuchangia na kujifunza kwa pamoja. Hatua yoyote ya kuimarisha vyama vyetu ni hatua ya kuimarisha demokrasia ya taifa letu.

Naomba nitoe rai kwa vyama vyote kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Msajili si kama mlezi na msimamizi tu, bali kama mshirika wa maendeleo ya kisiasa nchini. Tunahitaji vyama madhubuti, vinavyotii sheria, vinavyoendeshwa kwa uwazi na vinavyowajibika kwa wanachama wao na jamii kwa ujumla.

Kwa haya machache, natamka kuwa mafunzo haya yamefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza.